

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI
DAR ES SALAAM**

MATANGAZO YA DOMINika YA 32

MWAKA C TAREHE 06 NOVEMBA, 2022.

Kristo...

MCHANGO WA PILI

Kwa ajili ya **UJENZI WA OFISI**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

USHEMASI

Shirika la Warosmini wanawatangaza kuwa Frateri Severine Onesphory Kilala, IC mzaliwa wa Moshi, Parokia teule ya Mt. Martin De Pores. Ni mtoto wa Onesphory Kilala na Aloicia Paul Tarimo.

Frateri Mathias Hamenyimana Misibo, IC mzaliwa wa Kaliua, Tabora, Parokia ya Mt. Anthony wa Padua mtoto wa Thomas Misibo na Agnes Chubwa.

Wanategemea kupewa daraja Takatifu la Ushemasi tarehe 16 Novemba 2022 katika Parokia ya Ekaristi Takatifu Lushoto.

Tangazo la Tatu na la mwisho.

Tuwaombee ili waweze kufika daraja hilo wanadolitamani.

NDOA

BW. Kalla Msigwa mtoto wa Meji Galamgendela na Fridah Urasa na Bi. Jesca Msheku mtoto wa Leons Stambuli na Bibiana Mwanamshiki.

Tangazo la Tatu na la mwisho

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

SIKU YA MAVUNO KIJIMBO

Siku ya mavuno Kijimbo itaadhimishwa tarehe 19 Novemba 2022 Msimbazi Centre. Kutakuwa na adhimisho la Misa Takatifu ya shukrani itakayoanza saa 3:00 Asubuhi. Waumini wote mnaalikwa kuhudhuria Misa hiyo.

Viongozi wa Jumuiya mnaombwa kuonana na uongozi wa Parokia mara baada ya Misa.

TANGAZO LA WAWATA

Kutakuwa na Misa ya Shukrani ya WAWATA Dominika ya tarehe 13/11/2022 ikifuatiwa na maonyesho ya ujasilia mali kama tulivyo zoea. Wajasiriamali watakaoshiriki wajiorodheshe majina kupitia viongozi wa wawata Jumuiya na kundi la ujasiriamali. Waumini wote tunaalikwa kushiriki tukio hilo. Vazi la siku hiyo ni

kitenge cha Mt. Maria de Mattias. Vitenge vipo duka la wawata na vimepunguzwa bei kutoka sh. 27,000 mpaka 15,000 nyote mnakaribishwa.

UTOTO

Kutakuwa na Ibada ya kuhitimisha Jubilei ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa Utoto Mtakatifu Kiparokia itafanyika tarehe 26/11/2022. Kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu ikifuatiwa na michezo mbalimbali itakayoandaliliwa kikanda na baadae kutakuwa na chakula cha Pamoja kwa Watoto na walezi wao. Washindi watapewa zawadi. Tunaomba ushirikiano kutoka kwa wazazi. Mazoezi ya michezo yatafanyika hapa Parokiani.

UCHAGUZI

Kanda za Bethlehem, Kana na Nazareti watafanya uchaguzi leo mara baada ya misa hii ya kwanza, walengwa ni viongozi watano wa Kamati Tendaji za Jumuiya. Viongozi wa Kanda mnaombwa kutoa ushirikiano wa mahali ambapo uchaguzi utafanyika.

TEGEMEZA JIMBO

Viongozi wa Jumuiya ambazo bado hawajakamilisha mchango wa Tegemeza Jimbo waonane na Kamati Tendaji mara baada ya Misa kuangalia namna ya kukamilisha mchango huo.

UJENZI WA OFISI

Plasta inamaliziwa.

UTARATIBU WA NIA ZA MISA

Mwisho wa kupokea Nia za Misa ni Jumamosi saa nne na Nusu, ili ziweze kuandaliwa vizuri. Nia za Misa zitakazoletwa Zaidi ya hapo zitasomwa wiki inayofuata

HUDUMA KANISANI

Dominika hii tulihudumiwa na Jumuiya ya Mt. Anthony wa Padua Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya WAWATA Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Marko Mwinjili wajiandae.

MAUZO

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu. Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem.